

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI

S.L.P. 9121

Arauni ya Simu ***ELIMU DAR ES SALAAM
SIMU 116146-82
Tele: 41742 Elimu Tz
Fax: 13271 Elimu Tz
Unapojibu tafadhali tuju:



DAR ES SALAAM

Kumb.Na.ED/OK/C.2/III/116

Tarehe: 27/11/2002

Makatibu Tawala wa Mikoa
Wakaguzi Waaku wa Shule wa Kanda
TANZANIA BARA

WARAKA WA ELIMU NA. 24 WA MWAKA 2002

KUHUSU ADHABU YA VIBOKO

Inategemewa kuwa kila mwanafunzi anayeandikishwa shule atahudhuria mpaka analize elimu ngazi aliyoandikishwa. Vilevile mwanafunzi anapokuwa shule anatazamiwa kufuata sheria za shule ili kumwezesha kufuata masomo yake. Hata hivyo wako baadhi ya wanafunzi ambao ni watovu wa nidhamu hata kusababisha walimu kuchukua hatua za kinidhamu, Hatua hizo ni pamoja na adhabu ya viboko.


Adhabu ya viboko inaweza kutolewa kwa utovu wa nidhamu uliokithiri au kwa makosa ya jinai yaliyotendeka shuleni au nje ya shule yanayolitea kutoa adhabu hii:

- Adhabu itazingatia ukubwa wa kosa, umri, jinsi na afya ya mtoto na isizidi viboko vingine kwa wakati mmoja.
- Adhabu ya viboko itatolewa na Mwalimu Mkuu au Mwalimu mwingine atakayeteuliwa na Mwalimu Mkuu kwa maandishi, kila mara kosa linalostahili adhabu hii linapotendeka.
- Mwanafunzi wa kike atapewa adhabu ya viboko na mwalimu wa kike tu isipokuwa kama shule haina mwalimu wa kike.
- Kila mara adhabu ya viboko inapotolewa adhabu iorodheshwe katika kitabu kilichotengwa kwa kusudi hili ikiwa ni pamoja na - jina la mwanafunzi aliyepewa adhabu, - kosa alilotenda, - Idadi ya viboko na - jina la mwalimu aliyetoa adhabu hiyo.
- Mwalimu Mkuu atie saina katika kitabu kila mara adhabu hii inapotolewa.

- Mwanafunzi au mzazi akikataa adhabu ya viboko atasimamishwa shule.
- Hatua za kindhamu zitachukuliwa kwa mwalimu yeyote ambaye atakiuka utaratibu wa adhabu ya viboko.

Kwa Waraka huu ijulikane kuwa ni marufuku kwa mwalimu yeyote kuonekana na fimbo mikononi kwa lengo la kumwadhibu mwanafunzi.

Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Desemba 2002.



R.A. Mpama

KAIMU AFISAE LIMU KIONGOZI